# TAARIFA YA MKOA WA KIGOMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI YA MWAKA 2015 – 2020 KATIKA KIPINDI CHA MWAKA MMOJA KUANZIA MWEZI JUNI MWAKA 2020 HADI JULAI, 2021

## 1.0 Utangulizi

Taarifa hii inaelezea Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020 kwa kipindi cha mwaka mmoja. Katika kipindi hiki hatua kubwa ya utekelezaji imefanyika na mafanikio makubwa yameonekana katika Sekta mbalimbali.

Mkoa unaendelea kuhamasisha zao la Michikichi ambapo kwa sasa eneo linalolimwa zao hilo Mkoani Kigoma ni hekta 23,112. Kati ya eneo hilo hekta 19,556 zimepandwa miche ya zamani aina ya Dura (jiwe) na hekta 3,556 zimepandwa miche bora aina ya Tenera ipatayo 450,646.

Mtandao wa Barabara Vijijini na Mijini Mkoani Kigoma wenye jumla ya urefu wa Km 4,812.98 umeendelea kuboreshwa chini ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA). Kati ya Kilomita hizo, Km 2,129.47 ni barabara za mjazo (Feeder roads), Km 2,161.80 ni barabara za Mkusanyo (Collector roads) na Km 328.24 ni barabara za Jamii (Community roads). Aidha, Mkoa una Barabara za ndani za lami zenye urefu wa Km 65.129 zilizojengwa katika Halmashauri ya Mji Kasulu Km 4.919, Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo Km 1.86, Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji Km 45.44, Halmashauri ya Uvinza 10km, Halmashauri ya Kakonko 1km na Halmashauri ya Buhigwe 1.9km. Miradi ya ujenzi wa barabara katika Halmashauri zote itaendelea kutekelezwa kwa kiwango cha lami kupitia bajeti ya miradi ya maendeleo. Takwimu hizi ni kwa mujibu wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA).

Aidha, huduma za Afya zimeendelea kuboreshwa katika Halmashauri zetu Mijini na Vijijini kwa kujenga Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati. Uboreshaji huu unahusisha pia Halmashauri nne (4) zilizoanzishwa kutoka Halmashauri Mama. Katika Halmashauri 4 zilizoanzishwa, Halmashauri tatu (3) zinajengwa Hospitali za Wilaya na Halmashauri moja inajenga Zahanati katika kipindi hiki. Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Juni 2021 ilipokea Shilingi 1,500,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambao unaendelea kwa kutumia *Force Account*. Ujenzi huu unahusisha majengo mawili (2) ya Wagonjwa wa nje (OPD) na Maabara. Majengo hayo yapo katika hatua ya umaliziaji. Vile vile, Halmashsuri ya Wilaya ya Buhigwe ilipokea 500,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Wodi ya akinamama, Watoto na Wanaume katika Hospitali ya Wilaya. Katika Mtaa wa Jitegemee Kata ya Mwilamvya Tarafa ya Heruchini, Halmashauri ya Mji Kasulu inaendelea kukamilisha ujenzi wa Zahanati kwa gharama ya Shilingi 50,000,000/= jengo limefikia hatua ya kupaua. Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza imejenga pia Hospitali ya Wilaya katika Makao Makuu ya Halmashauri kwa gharama ya Shilingi 2,300,000,000/= na kwa sasa Hospitali imeanza kutumika. Jengo linaloendelea kujengwa ni Wodi ya Watoto na Wanaume ambayo imefikia hatua ya msingi.

Taarifa hii ina sehemu kuu 6, Sehemu ya kwanza ni Utangulizi na imeelezea mambo makubwa yaliyofanyika katika kipindi hiki cha utekelezaji. Sehemu ya pili inaelezea utekelezaji uliofanyika kisekta, Sehemu ya tatu inaelezea kwa muhtasari mafanikio yaliyopatikana kisekta kwa mwaka mmoja hadi Juni, 2021 Sehemu ya nne inaelezea changamoto zilizojitokeza na utatuzi wake wakati Sehemu ya tano inaelezea mipango/miradi inayotekelezwa na itakavyotekelezwa katika kipindi kifupi kijacho. Sehemu ya sita ni hitimisho.

## 2.0 Utekelezaji wa Ilani Kisekta

### 2.1 SEKTA YA UZALISHAJI MALI

#### 2.1.1 KILIMO NA USHIRIKA

**Bangokitita Na.2.1.1:**

| IBARA | MAELEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 22(a) | Kuimarisha upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo ili kuongeza tija na uzalishaji kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia ya kisasa hususani katika kuboresha mifumo ya utoaji wa ruzuku na pembejeo pamoja na kuwaunganisha wakulima na Benki ya Maendeleo ya Kilimo na taasisi nyingine za fedha. | Mkoa unaendelea kuhimiza matumizi ya zana bora za kilimo kama matrekta na utumiaji wa "wanyamakazi" katika kilimo. Kwa upande wa matumizi ya matrekta, Halmashauri zimeanza utaratibu wa kuanzisha vituo vya kukodisha matrekta kwa ajili ya kilimo. Halmashauri zilizoanzisha hadi sasa ni Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza (vituo 3) na Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko (kituo 1). Kwa upande wa wanyamakazi, kwa sasa kuna jumla ya jozi za maksai 601; Wilaya ya Uvinza 522, Wilaya ya Uvinza 60, Kibondo 16, Kakonko 3). |
| 22(b) | Kutoa elimu kwa wakulima juu ya kanuni bora za kilimo katika kila Kata nchini. | Elimu kuhusiana na Kanuni bora za kilimo hutolewa na Mkoa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Maendeleo katika kilimo hususani Mradi wa Kilimo endelevu Mkoa wa Kigoma (SAKIRP), Shirika la Chakula Duniani (WFP) na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Taifa (FAO). Jumla ya vikundi vya wakulima 812 vyenye jumla ya wakulima 18,371 wamepewa elimu na mafunzo. Aidha, Mkoa utaendelea kushirikiana na wadau hao ili kuhakikisha wakulima wanaongeza uzalishaji kwa kutumia mbinu bora za kilimo cha kisasa. |
| 22(c)(i) | Kushirikiana na sekta binafsi, kuwekeza katika miundombinu ya umwagiliaji kwa kujenga mifereji mikuu, mifereji ya kati na kujenga mabwawa ya kuhifadhia maji kwenye maeneo yenye ukame. | Kwa hivi sasa hakuna fedha iliyopokelewa kwa ajili ya ujenzi wa mifereji Mikuu, mifereji ya kati na mabwawa. Aidha, Mwaka 2019 ilijengwa mifereji katika eneo la Mgela lenye ukubwa wa hekta 360 kwa gharama ya Shilingi 168,000,000/= kwa ufadhili wa Benki ya Dunia (World Bank). |
| 22(c)(ii) | Kukamilisha ujenzi wa skimu zote za umwagiliaji zilizoanza kujengwa miaka ya nyuma. | Mkoa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu na Halmashauri ya Wilaya ya |

| | | |
|---|---|---|
| | | Uvinza zilipata jumla ya Shilingi 1,176,000,000 kutoka Programu ya "Small Scale Irrigation Development Programme" (SSIDP) kwa ajili ya uboreshaji wa Miundombinu ya Miradi ya Umwagiliaji minne (4). Skimu hizo ni Rungwe Mpya Shilingi 349,000,000/=, Titye Shilingi 230,000,000/=, Kashagulu Shilingi 340,000,000/= na Ruhwiti Shilingi 257,000,000/=. Ujenzi na ukarabati wa Miundombinu ya Miradi hii ya umwagiliaji imekamilika. |
| 22 (g) (iii) | Kujenga masoko ya kimkakati katika maeneo ya mipaka ya nchi ili kuwapa wakulima fursa ya kuuza mazao nje ya nchi. | Jumla ya masoko na vituo vya kukusanyia na kuuza mazao 5 vimejengwa kwa ushirikiano baina ya Serikali na Wadau wa Maendeleo hususani ITC na UNCDF. Vituo na masoko hayo ni Muhange na Kabingo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kakono, Kagezi na Mukarazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo na Mvugwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu. Ni matarajio ya Mkoa kuwa vituo na masoko haya yatatoa fursa kubwa na ya uhakika wakulima kuuza mazao yao nje ya nchi. |

### 2.1.2 MIFUGO NA UVUVI

Bangokitita Na.2.1.2:

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 25(b) | Kutenga, kupima na kumilikisha wafugaji maeneo ya ufugaji nchini ili kuongeza maeneo ya ufugaji yaliyopimwa. | Kwa mujibu wa takwimu kutoka baadhi ya Halmashauri, mwaka 2020 jumla ya maeneo 20,186 yalitengwa na kupimwa. Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe maeneo 5, Kakonko maeneo 7, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu maeneo 17,182, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma maeneo 2955, Uvinza maeneo 37. Aidha, kwa mwaka 2021 Mkoa kupitia Halmashauri umepanga kutenga na kupima maeneo 3047 (Kasulu TC maeneo 2, Buhigwe DC maeneo 44, Kakonko DC maeneo 2, Kigoma DC maeneo 3,000 na Uvinza DC maeneo 37). |
| 25 (p) | Kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha viwanda vya nyama na mazao mengine yatokanayo na mifugo ikiwemo jibini na ngozi hususan katika maeneo yenye mifugo mingi ili | Serikali inaendelea kuhamasisha Sekta binafsi kuanzisha viwanda vidogo vya nyama katika maeneo yenye mifugo |

| | | |
|---|---|---|
| | kuongeza thamani. | mingi (Uvinza, Kasulu, Kibondo) ili yaweze kuchakata mazao ya mifugo kama ngozi na jibini. |
| 27 (n) | Kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo kupata vifaa vya uvuvi kwa bei nafuu. | Katika mwaka 2020/2021 Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza chini ya Ufadhili wa Marekani kupitia kikundi cha "The Nature Conservant" (Tuungane) ilitoa kiasi cha Shilingi 45,000,000/= kwa ajili ya miradi mitatu (3) ya vifaa vya uvuvi. Mradi wa Ununuzi wa chombo cha uvuvi (KIPE) – Kaparamsenga, Mradi wa Ununuzi wa chombo cha uvuvi (KIPE) – Kalya na Mradi wa Duka la kuuza betri za kuchajia taa za wavuvi wadogo wadogo – Mgambo. |
| 27 (p) | Kuendelea Kupambana na Uvuvi haramu ili uvuvi uwe endelevu na wenye tija. | Doria zimeendelea kufanyika ili kudhibiti uvuvi haramu. |

### 2.1.3 UTALII NA MALIASILI

Bangokitita Na.2.1.3:

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 29 (b) | Kuongeza msukumo katika utalii wa maeneo ya kihistoria kwa kuboresha miundombinu kwenye maeneo ya malikale na kuyatangaza maeneo hayo. | Mkoa kwa kushirikiana na TANAPA umeboresha miundombinu kwenye maeneo ya malikale na kuyatangaza maeneo hayo kupitia vyombo vya habari na Mikutano ya Kimataifa. |
| 31 (e) | Kuendelea kuimarisha doria za ulinzi wa wananchi dhidi ya wanyamapori kwa kuboresha mfumo wa utoaji taarifa za wanyamapori waharibifu. | Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri na Waheshimiwa Wabunge/Madiwani na Wananchi umekuwa ukishughulikia taarifa zinazotolewa kwa kutembelea sehemu husika ambapo uharibifu umefanywa na wanyamapori hao. Taarifa hizi pia zimekuwa zikitolewa na Waheshimiwa Madiwani kupitia vikao vyao. Katika kikao cha Baraza la Madiwa Manispaa Kigoma/Ujiji kilichofanyika tarehe 25/02/2021ilitolewa taarifa kuhusu viboko kutembea ovyo na kusababisha athari kwa kuuwa baadhi ya watu wanaotembea pembezoni mwa Ziwa Tanganyika katika Kata za Kitongoni na Kagera. Pamoja na uongozi kutembelea eneo hilo, Mbunge wa kigoma Mjini Mhe. Ng'enda aliahidi kushughulikia suala hili ili likajadiliwe Bungeni kwa upana na hatua ziweze kuchukuliwa. Mkoa |

| | | |
|---|---|---|
| | | unaendelea kumshukuru Mhe. Mbunge kwa jitihada hizo. |
| 31 (f) | Kuongeza eneo la kupanda miti hadi hekta 130,000 mwaka 2020 na kuhakikisha kwamba mbao zinazovunwa zinatumiwa kwa ajili ya kutengeneza samani na matumizi mengine hapa nchini badala ya kusafirisha magogo nje ya nchi. | Kwa mwaka 2020/2021 Mkoa kwa kushirikiana na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na wadau wengine umefanikiwa kupanda miti 3,549,633 na kuitunza kwa ajili ya kuongeza kipato cha wananchi. |

### 2.1.4 VIWANDA NA BIASHARA

Bangokitita Na.2.4:

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 33 (b) | Sekta ya Viwanda inaongeza ajira kwa kuweka kipau mbele cha kujenga viwanda vinavyotumia malighafi zinazozalishwa hapa nchini kama vile kilimo, mifugo, uvuvi na maliasili; Viwanda hivyo ni pamoja na viwanda vya nguo, sabuni, korosho, matunda n.k | Mkoak kupitia Halmashauri umeendelea kuwahamasisha wananchi na wadau wengine kuanzisha viwanda vinavyotumia malighafi ya ndani. Mkoa una ongezeko la viwanda vidogo 220 vinavyozalisha Sabuni, Mafuta ya Mawese na Muhogo. |
| 33 (c) | Kuandaa mikakati thabiti ya kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha viwanda vikubwa na vya kati nakuweka utaratibu wa kuvilinda dhidi ya viwanda vya nje. | Mkoa unaendelea kuwahamasisha wadau mbalimbali ili wawekeze katika viwanda ili kukuza uchumi Mkoani Kigoma. Aidha, kiwanda cha kuchakata mazao ya nyuki kimekamilika katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo. |
| 33 (g) | Kuendeleza kasi ya ujenzi wa viwanda vidogo na vya kati hasa vinavyosindika mazao. | Mkoa kupitia Halmashauri umeendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vidogo na vya kati vinavyosindika mazao ili kuongeza thamani ya mazao. Kwa sasa Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma unaendelea kukisimamia kiwanda cha KANYOVU kinachosindika kahawa ili kiendelee kuwa bora zaidi kwa kutoa kahawa bora. |

### 2.1.5 MADINI

Bangokitita Na. 2.1.5

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 35(m)(i) | Kuwatambua, kuwarasimisha na kuwapatia wachimbaji wadogo maeneo ya uchimbaji madini. | Wachimbaji madini wadogo 434 wenye leseni wametambuliwa. Takwimu hii ni ya Mkoa mzima. |
| 35 (n) | Kuendelea kuimarisha ukaguzi wa migodi katika masuala ya usalama, utunzaji wa mazingira na afya migodini | Ufuatiliaji umefanyika kwa kukagua Migodi yote 180 inayofanya kazi katika Mkoa. |

## 2.2 SEKTA YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA KIUCHUMI

### 2.2.1 ARDHI

Bangokitita Na. 2.2.1

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 37 (a) (vi) | Kufanya uhakiki wa mashamba pori yasiyo endelezwa kwa kipindi kirefu na kugawa upya kwa wananchi | Uhakiki wa mashamba pori yasiyoendelezwa umefanyika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu (mashamba 5) na Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza (mashamba 11). |
| 37 (a) (viii) | Kutoa elimu kwa umma juu ya Sheria za Ardhi, Sheria ya Mipangomiji, Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na Sheria zingine zinazohusiana na utawala wa ardhi | Halmashauri zote nane za Mkoa zimefikiwa na kupewa ushauri. |
| 37 (b) (ii) | Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya Vijiji na Mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya | Vijiji 4 Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu na Vijiji 4 Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma vimeandaliwa Mipango ya Matumizi ya ardhi ya Vijiji katika kipindi hiki. |
| 37 (b) (iii) | Kukamilisha upimaji wa mipaka ya vijiji vyote nchini | Vijiji 8 vimepimwa mipaka ya Vijiji. Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu Vijiji 4 na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma Vijiji 4. |
| 37 (b) (v) | Kuwapatia wananchi hatimiliki pamoja na kusajili nyaraka nyingine za kisheria | Kwa mujibu wa takwimu kutoka Ofisi ya Kamishina Msaidizi wa Ardhi Mkoa Kigoma, jumla ya Hati miliki 2030 zimetolewa kwa kipindi hiki. |

### 2.2.2 USAFIRI NA UCHUKUZI

Bangokitita Na.2.2.2

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 39 (b) (ii) | Kuhakikisha kuwa makao makuu ya Wilaya ambazo bado barabara zake hazipitiki majira yote zinafanyiwa ukarabati angalau kwa kiwango cha changarawe na kuzifanya zipitike majira yote ya mwaka. | Barabara zimeendelea kufanyiwa ukarabati mara kwa mara kutokana na fedha zinazotengwa na kutolewa katika bajeti ya kila mwaka na hali ya barabara inaridhisha. |
| 39 (b) (iii) | Kupunguza Umaskini kwa kushirikisha kikamilifu vikundi vya wananchi katika kazi za matengenezo madogo madogo ya barabara kama vile kazi za kufyeka nyasi, kuzibua mifereji na kufanya usafi wa barabara zinazopita katika maeneo yao. | Kampuni zinazojishughulisha na ujenzi wa Barabara zimeshauriwa kushirikisha vikundi vilivyosajiliwa kisheria kwenye ujenzi wa barabara hasa matengenezo madogo madogo. |
| 39 (c) (i) | Kukamilisha ukarabati wa barabara zote unaoendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami ambao umekwishaanza katika barabara kuu na barabara za Mikoa | Barabara za lami zilizojengwa katika Barabara Kuu ni km 281.08 kati ya km 375.41 za Barabara za Changarawe/Udongo. Aidha, barabara za Mkoa za Mkoa zenye urefu wa km |

| | | |
|---|---|---|
| | | 729.87 bado hazijaanza kutekelezwa. |
| 39 (d) (i) | Kuanza ujenzi mpya na ukarabati wa barabara kwa kiwango cha lami | Katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya Mikataba 42 yenye thamani ya Shilingi 16,472,022,000/= ambayo inahusisha matengenezo ya Barabara kuu, Barabara za Mkoa na ujenzi wa madaraja zimefanyiwa manunuzi. Aidha, jumla ya Mikataba yenye jumla ya Shilingi 16,193,348,000/= imeshasainiwa na kiasi kilichobaki kipo katika hatua ya manunuzi. Baadhi ya wakandarasi wanaendelea na kazi baada ya kupata msamaha wa kodi. |

### 2.2.3 USAFIRI WA MAJINI

Bangokitita Na. 2.2.3:

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 41 (h) | Kuendelea na uboreshaji wa miundombinu ya bandari za Ziwa Nyasa na Tanganyika ili kuimarisha huduma zitolewazo kwa kujenga magati ya Kagunga, Kasanga, Kibirizi, Itungi na Kiwira | Kama ilivyoelezwa katika taarifa zilizopita mradi ulianza kutekelezwa mwezi Agosti, 2015 na ulikamilika Januari, 2017. |

### 2.2.4 USAFIRI WA ANGA

Bangokitita Na. 2.2.4:

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 41 (d) | Kujenga na kukamilisha awamu ya pili ya Viwanja vya Ndege vya Tabora na Kigoma | Miradi ya ujenzi wa Viwanja vya Ndege inasimamiwa na Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa Kigoma chini ya Ufadhili wa European Investment Bank). Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na;-<br>a. Ujenzi wa jengo la abiria<br>b. Ujenzi wa sehemu ya maegesho<br>c. Ujenzi wa njia za ndege (Tax ways).<br>d. Ujenzi wa mnara wa kuongozea ndege (control tower)<br>e. Ujenzi wa taa za kuongozea ndege wakati wa usiku.<br>f. Ujenzi wa jengo la zima moto<br>g. Barabara za kuingia na kutoka uwanja wa ndege (Access roads to Airport).<br>Wakala wa Barabara (TANROADS Mkoa Kigoma) imewasilisha nyaraka za Tenda (Tender Documents) kwa mfadhili ili aweze kutoa idhini. Majibu bado hayajatolewa na mfadhili. |

### 2.2.5 NISHATI

Bangokitita Na.2.2.5

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 43 (c) | Kuendelea kusambaza umeme wenye uhakika mijini na vijijini | Serikali imeendelea kusambaza umeme kwa wananchi wanaoishi Mijini na Vijijini. Kwa mujibu wa takwimu kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa Kigoma, idadi ya wananchi waliounganishiwa huduma ya Umeme Mijini na Vijijini kuanzia mwezi Juni, 2020 hadi Juni, 2021 ni 10,529. Aidha, Vijiji 92 vimeunganishiwa huduma ya umeme katika kipindi hiki. |

## 2.3 SEKTA YA HUDUMA ZA JAMII

### 2.3.1 AFYA

Bangokitita Na. 2.3.1

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 50 (a) (i) | Kuhakikishalengo la kila kijiji kuwa na Zahanati,Kata kuwa na Kituo cha Afya na Wilaya kuwa na Hospitali linaendelea kutekelezwa katika maeneo ambayo huduma hizi hazijakamilika pamoja na kujenga hospitali za wilaya katika wilaya zote mpya. | Serikali ilitoa fedha kiasi cha Tsh. 6,420,000,000 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya upanuzi wa miundombinu ya huduma za Afya na uboreshaji wa huduma za upasuaji wa dharura katika vituo vya huduma 14, (vituo vya Afya 13 na Hospitali 1) kwa awamu nne katika Halmashauri za wilaya ya Kigoma, Uvinza, Kasulu, Buhigwe, Kibondo, Kakonko pamoja na Hospitali ya Halmashauri ya Mji Kasulu. Miradi hii imekamilika na huduma zinatolewa. |
| 50 (b) (i) | Kuwagawia wananchi vyandarua vyenye viuatilifu bila malipo. | Kiwango cha utoaji wa vyandarua kwa mama wajawazito kimeendelea kuongezeka ambapo kwa mwaka 2020 jumla ya akina mama wajawazito 116,402 walipata vyandarua vyenye kiuatilifu cha muda mrefu sawa na asilimia 93 ukilinganisha na asilimia 82.7 kwa mwaka 2019 ambayo ni ongeeko la asilimia 10.3 (10.3%). |

| | | |
|---|---|---|
| 50 (b) (ii) | Kutekeleza mpango wa upuliziaji wa viuatilifu ukoko katika kuta za nyumba ili kuua mbu wanaoeneza malaria katika Mikoa ya Kigoma na Lindi | Mwaka 2020, Mkoa ulitumia lita 5200 kutekeleza zoezi la unyunyiziaji wa viuadudu vya kibailojia kwenye mazalia ya mbu. Jumla ya mazalia yenye mita za mraba 1508905 ambapo jumla ya mazalia 496703 yalinyunyiziwa sawa na asilimia 32. Aidha, Kaya 189,852 zilipuliza viuatilifu ukoko katika kuta za nyumba. |
| 50 (b) (iv) | Kununua na kusambaza dawa za malaria katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya | Vituo vyote vya huduma katika Mkoa vinatoa tiba ya malaria kwa dawa za mseto kwa malaria isiyo kali na artesunate na/au Quinine kwa malaria kali. Kwa mwaka 2020, Dawa hizi zimekuwa zikipatikana kwenye vituo vya kutolea huduma kwa wastani wa asilimia 98.8%. Upatikanaji wa dawa za SP kwa ajili ya mama wajawazito umeimarika na dawa hizi zimekuwa zikipatikana kwa wastani wa asilimia 95. Upatikanaji wa vitenganishi vya kipimo cha haraka cha MRDT kwenye vituo vya kutolea huduma ni wastani wa asilimia 98. |
| 50 (j) | Kuweka utaratibu utakaowawezesha wananchi kuwa na Bima ya Afya ili kumudu gharama za matibabu | Hadi kufikia Desemba, 2020 jumla ya Kaya 3469 zilisajiliwa katika Mfuko huu. Jitihada zinaendelea za kuwahamasisha wananchi ili waweze kujisajili zaidi. |

### 2.3.2 ELIMU

Bangokitita Na. 2.3.2

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 80 (a) | Kujenga na kukarabati miundombinu ya elimu pamoja na kuhifadhi na kuendeleza mazingira ya shule hizo. | Vyumba vya madarasa vilivyojengwa katika shule za msimgi vimefikia 2095. Idadi ya vyumba vya madarasa vilivyojengwa katika shule za Sekondari ni 1018. Aidha, fedha inayolipwa ya wanafunzi wanaonufaika na Mpango wa Elimu bila malipo ni 3,563,836,301/=. |
| 80 (c) | Kuimarisha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum | Kwa mwaka 2020 idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu waliopata fursa |

| | | |
|---|---|---|
| | | ya elimu imefikia 1032. |
| 80 (h) | Kuimarisha ufundishaji wa masuala yote mtambuka katika ngazi zote za elimu, ikijumuisha UKIMWI/VVU, mabadiliko ya hali ya hewa, utunzaji wa mazingira, masuala ya jinsia n.k. | Kwa mujibu wa Halmashauri, idadi ya Walimu waliojengewa uwezo juu ya masuala mtambuka imefikia 452. |

### 2.3.3 MAJI

Bangokititа Na. 2.3.3

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 54 (a) | Kuboresha huduma ya maji Vijijini kutoka asilimia 67.7 mwaka 2015 hadi asilimia 85 mwaka 2020 (lengo la kitaifa) | Mkoa unaendelea na ukamilishaji wa miradi ya maji iliyoanza kutekeleza katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ili iweze kufikia asilimia 80. |
| 54 (b) (ii) | Kuongeza upatikanaji wa huduma za maji katika miji mikuu ya Mikoa kutoka asilimia 86 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 95 mwaka 2020 (lengo la kitaifa) | Serikali imeendelea kuboreresha huduma ya maji katika Halmashauri zetu. Mfano, Wananchi wa Manispaa Kigoma/Ujiji wanatumia lita milioni 20 za maji kwa siku. Aidha, Mpango wa Serikali ni kuongeza lita za maji hadi kufikia lita milioni 42 kwa siku. Aidha, mahitaji ya sasa ya maji ni lita milioni 23. |
| 54 (b) (iii) | Kuongeza upatikanaji wa huduma za maji katika miji mikuu ya Wilaya, miji midogo na maeneo ya miradi ya Kitaifa kutoka asilimia 57 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 90 mwaka 2020 (lengo la kitaifa) | Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi haraka ya maji katika Halmashauri ili kuhakikisha maji yanapatikana kwa wingi. Kazi hiyo imefanyika katika miji ya Kakonko, Buhigwe na Uvinza. |

## 2.4 MAENEO MENGINE MUHIMU

### 2.4.1 KUENDELEZA MAKUNDI MAALUM

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 165 (a) | Kuhakikisha wazee wanatambuliwa na kupatiwa huduma za matibabu | Katika kila kituo cha kutolea huduma za Afya wazee hupewa kipaumbele katika kupatiwa huduma za Afya. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 wazee 59,051 (wanawake 34,272 na wanaume 24,779) wametambuliwa na kupewa vitambulisho vya matibabu. |
| 165 (b) | Kuhakikisha wazee wanapata haki zao za kisheria na kupata fursa sawa katika ngazi zote | Mkoa umeendelea kusimamia haki za Wazee kwa kuwashirikisha katika vikao vya Mabaraza ya Madiwani na kupewa fursa ya kutoa ushauri/maoni. |

### 2. 4. 2 WATU WENYE ULEMAVU

Bangokitita Na. 2.4.1

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 63 (a) | Kuendelea kuwapatia Mikopo yenye masharti nafuu, elimu ya ujasiriamali na biashara vikundi vya Wanawake na Vijana ili kuwawezesha kuongeza ajira, ujuzi wa kujiajiri, fursa za kipato na kujikimu. | Kila Halmashauri hutenga na kutoa fedha kwa ajili ya Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Juni, 2021 jumla ya Shilingi 1,001,319,607.65/= zilitengwa kwa ajili ya mikopo ya vikundi 154 vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Aidha, katika kipindi hicho Shilingi 835,466,722.83/= zilitolewa kwa vikundi hivyo sawa na asilimia 83.4. |
| 166 (a) | Kuhakikisha kwamba Walemavu wote nchini wanaendelea kutambuliwa na kulindwa na vitendo vinavyoshusha utu vikiwemo ubaguzi, uonevu, ukatili na mila potofu. | Mkoa kupitia Halmashauri zetu umefanikiwa kuanzisha Kamati za watu wenye ulemavu ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanakuwa na fursa sawa katikajamii. |
| 166 (b) | Kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wa ngozi (albino) wanalindwa dhidi ya ukatili na ubaguzi wa aina yoyote. | Mkoa kwa kushirikiana na Wadau umeendelea kuzisimamia kliniki maalum za matibabu zilizoanzishwa katika Halmasahuri za Kibondo, Kasulu na Kigoma. Kliniki hizo hutoa vipimo vya vimelea vya Kansa, Kutoa matibabu ya ngozi na kofia kwa ajili ya kujikinga na jua. |

## 3.0 Muhtasari wa Mafanikio yaliyopatikana Kisekta

Katika kipindi cha mwaka mmoja (Juni, 2020 – Julai, 2021) ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 – 2020 mafanikio yaliyopatikana Kisekta katika Mkoa wa Kigoma ni pamoja na;

### 3.1. Kilimo na Ushirika

- Mkoa kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo katika Kilimo wanashirikiana katika kuelimisha na kuwahamasisha wakulima juu ya umuhimu wa kutumia pembejeo bora za kilimo. Kwa msimu wa kilimo 2019/2020 jumla ya tani 49,246 za mbolea zilitumika ambapo kwa msimu wa 2020/2021 mahitaji ya mbolea yaliongezeka hadi kufikia tani 59,446 sawa na ongezeko la asilimia 9.3.

- Mkoa una vyama vya msingi vya Kahawa 14 katika Wilaya tatu (3) ambazo ni Kigoma (vyama 5), Buhigwe (vyama 8) na Kakonko (chama 1). Vyama vya msingi vya Tumbaku vipo 49; Wilaya ya Kakonko 2, Uvinza 33, Kasulu 10, Kibondo 4. Vyama vya msingi vya wakulima vya mazao mchanganyiko (Biashara na Chakula) vipo 10; Wilaya ya Kakonko vyama 4, Kibondo 2 na Kasulu 4 na AMCOS za zao la

chikichi zipo 10; Wilaya ya Kigoma 8 na Wilaya ya Uvinza 2. Aidha, Halmashauri zote zimeelekezwa kutenga bajeti kwa ajili ya kuhakikisha mazao haya ya kimkakati yanazalishwa kila mwaka.

- Aidha, Mkoa unaendelea kuongeza matumizi ya zana bora za kilimo yakiwemo matrekta ya kulimia yakiwa na vifaa vyake na matrekta ya kupandikiza mpunga. Utekelezaji unafanyika kupitia Halmashauri ambapo kila Halmashauri imeanza kuchukua hatua za kuanzisha vituo vya kukodisha matrekta ya kukodi. Halmashauri mbili zimeonesha mafanikio, Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko imeanzisha kituo katika

  Kijiji cha Kinonko na Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza imeanzisha vituo 3 katika vijiji vya Malagarasi, Kalya na Lugufu.
- Mkoa kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi Tanzania Kambi ya Bulombora Mkoani Kigoma utashughulikia suala la kilimo cha zao la Mchikichi eneo la Bulombora kwa kuomba Askari takribani 1000 ili watumike katika kilimo hicho badala ya kuwategemea wadau wanaojitolea (*Volunteers*) ambao hukaa kwa muda mfupi na kuondoka.

## 3.2 Ardhi

- Mkoa umeendelea kupima maeneo na kutoa Hati miliki. Kwa mwaka 2020 vimepimwa viwanja 12,764. Aidha, kwa mujibu wa Taarifa kazi za Upimaji maeneo Mkoa Kigoma kwa kipindi cha mwezi Juni, 2020 hadi Aprili, 2021 jumla ya maeneo 10,052 yalipimwa. Kigoma/Ujiji MC maeneo 6778, Kigoma DC 16, Kasulu DC 808, Kasulu TC 1221, Kibondo DC 768, Kakonko DC 174, Buhigwe DC 1 na Uvinza DC 286.

## 3.3 Usafirishaji na Uchukuzi (Miundombinu)

- Hali ya bararabara Mkoani ni nzuri kutokana na matengenezo mbalimbali yaliyofanyika kwa kutumia fedha za *roll over* 2019/2020 na yanayoendelea kufanyika mwaka wa fedha 2021/2022. Matokeo ya utekelezaji huo ni kuendelea kuimarika zaidi kwa mtandao wa barabara Mkoani Kigoma. Uimara wa mtandao huo umewezesha na kurahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa na abiria na kupunguza usumbufu kwa watumiaji wa barabara na hata nauli kushuka.

- Kwa kuzingatia ajira ya Vijana kwenye sekta ya Miundombinu ya barabara, vijana 874 wameajiriwa kwa muda katika miradi mitano (5) ya barabara zinazoendelea kujengwa Mkoani Kigoma. Barabara ya Kasulu – Manyovu Km 62.25 vijana 106 (wanawake 7, wanaume 99), Barabara ya Kanyani Mvugwe Km 70.5 vijana 302 (wanawake 24, wanaume 278), Barabara ya Mvugwe – Nduta Km 59.35 vijana 157, (wanawake 20, wanaume 137), Barabara ya Nduta – Kabingo Km 62.5 vijana 170 (wanawake 14, wanaume 156), Barabara ya Nduta – Kibondo (town link) Km 25.9 vijana 139 (wanawake 15, wanaume 124). Aidha, kwa sasa Mkoa kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa Kigoma umeshughulikia suala la *Complementary Projects* ambapo kwa sasa miradi hiyo ipo katika hatua ya manunuzi.

- Pamoja na hayo, Mkoa utaendelea kufuatilia Wizara ya Ujenzi fedha za ujenzi wa barabara yenye urefu wa Km 6 Wilayani Kibondo zilizoahidiwa na Mhe. Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Pombe Magufuli ili zitolewe kwa ajili ya ujenzi wa barabara na Mkandarasi alipwe fedha kwa wakati. Ufuatiliaji utafanyika pamoja na ule wa Mkandarasi aliyejenga Mita 630 Wilayani Kakonko kati ya Kilomita 3 za barabara lakini hajalipwa hadi sasa. Kwa mujibu wa TARURA Wilaya ya Kakonko, mwezi Juni, 2021 Mkandarasi huyo amelipwa kiasi cha Shilingi 100,373,988.25/= kati ya Shilingi 380,000,000/= anazodai.

- Mkoa utaendelea kufuatilia kuhusu ujenzi wa daraja la Nyabigufa Kata ya Mkongoro ambalo limejengwa lakini halipitiki kutokana na kutokamilika kwa Barabara zinazokutana kwenye daraja hilo. Mkandarasi anayejengwa barabara hizo ameanza ujenzi katika Kata ya Nyarubanda kwa sababu Mkataba wa kazi ni mmoja. Aidha, Mkandarasi alipewa Mkataba wa miezi mine (4) kuanzia mwezi Aprili, 2021 hadi mwezi Agosti, 2021.ili aweze kukamilisha kazi hizo.

- Maeneo mengine ambayo Mkoa utayafanyia ufuatiliaji ni pamoja na kuwasiliana na TARURA Wilaya ya Uvinza kuhusu suala la ujenzi wa matoleo ya vivuko vya kutoka kwenye barabara ya lami kwenda kwenye nyumba za wananchi wanaoishi maeneo ambako barabara inapita, kukumbushia Maagizo ya Mhe. Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Pombe Magufuli katika miradi ya ujenzi wa barabara Mkoani Kigoma.

- Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) katika Mkoa wa Kigoma imeendelea kuhudumia mtandao wa Barabara wenye urefu wa km 4,812,98. Mtandao huu utaendelea kuwa na mabadiliko kutokana na Wananchi kupitia Wakurugenzi wa Halmashauri kuendelea kuibua barabara zinazopaswa kuhudumiwa na TARURA.

- Mipango Kabambe ya kuboresha kiwanja cha Ndege cha Kigoma inaendelea kupitia ufadhili wa European Investment. Hadi sasa Nyaraka za Tenda zimewasilisha kwa mfadhili kwa ajili ya kupata idhini.

- Aidha, Mkoa utaendelea kushughulikia changamoto zilizopo na zinazoendelea kujitokeza katika maeneo mengine kwenye sekta ya Miundombinu Mkoani Kigoma.

### 3.4 Nishati ya Umeme

- Ili kukabiliana na changamoto ya upatikanaji umeme katika Mkoa wa Kigoma, ujenzi wa njia kubwa ya Umeme ya msongo wa Kilovolt 132 kutoka Tabora hadi Kigoma na kujenga kituo cha kupoozea umeme katika eneo la Urambo chenye ukubwa wa 35MVA na eneo la Nguruka chenye ukubwa wa 15MVA unaendelea. Hadi sasa ujenzi wa majengo katika vituo vya kupoozea umeme eneo la Nguruka tayari

umeshakamilika na mradi mzima unatarajiwa kukamilika August, 2023. Mradi huu unajengwa kwa fedha za ndani na unakadiriwa kugharimu jumla ya Shilingi Bilioni 69.

- Serikali inaendelea kuboresha huduma ya umeme kwa kuanza ujenzi wa njia kubwa ya umeme msongo wa 400kV kutoka Nyakanazi hadi Kigoma yenye urefu wa 280km sambamba na ujenzi wa kituo cha kupozea umeme Kidahwe. Kituo cha Kidahwe kitakapokamilika kitaboresha umeme katika maeneo yote ya Mkoa wa Kigoma na Wilaya zake. Utekelezaji wa mradi ni miezi 24 baada ya mkandarasi kusaini mkataba. Mradi huu unakadiriwa kugharimu dola za kimarekani (USD) milioni 168 hadi kukamilika kwake.

- Uthamini wa kuanza ujenzi wa Chanzo cha kuzalisha umeme wa Maji (Malagarasi Hydro) umefanyika na maeneo mbalimbali yatapitiwa na njia ya umeme. Kwa sasa utaratibu unaoendelea ni uhakiki wa uthamini kwenye njia itakayopita laini hiyo ya umeme ambapo pindi tuu uhakiki utakapokamilika taratibu za malipo kwa wathaminiwa zitaanza.

- Katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa umeme hivi sasa Kigoma tunapata umeme wastani wa 1MW kutoka kituo cha kuzalisha Umeme kwa kutumia nguvu ya jua. (Sola power plant), ambapo wanaendelea na maboresho ili kutupatia Umeme mwingi zaidi. Kituo hiki kwa sasa kinatupatia Umeme wakati wa mchana haswa kunapokuwa na mwanga wa jua wa kutosha.

- Kwa upande wa Wilaya ya Kasulu tayari mafundi wapo kazini kufunga mashine nyingine moja tofauti na zilizopo yenye uwezo wa kuzalisha 1.25MW ili kuongezea nguvu na kukabiliana na tatizo la umeme kwa Wilaya za Kasulu na Buhigwe kwa mashine itakayotoka Loliondo Ngorongoro.

- Mkoa utaenendelea kusimamia maeneo yaliyopimwa kwa ajili ya kupitisha umeme na kuwahizima wananchi ili waweze kuvuta umeme kwa gharama nafuu ya Shilingi 27,000/= kama Serikali ilivyoagiza. Pamoja na hilo, Mkoa utahakikisha wananchi hawafanyi shughuli zao chini ya nyaya za umeme wa njia kuu (High Voltage) ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza.

- Aidha, Mkoa kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) utafanya mazungumzo na Kampuni ya Nextgen Solarwaz ili kuhakikisha Kampuni hiyo inaongeza uzalishaji wa umeme sambamba na kumuomba Waziri wa Nishati ili aongeze Genereta mbili (2) za kufua umeme ili Mkoa uweze kupata huduma ya umeme hadi kufikia 5MW.

### 3.5 Afya

- Mkoa umeandaa Mpango wa Dharura wa miaka mitatu wa kukabiliana na vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga.

- Mkoa utaendelea na uhamasishaji ngazi ya jamii juu ya umuhimu wa kuanza Kliniki ya wajawazito mapema kwa kutumia wahudumu wa afya ya jamii waliopata mfunzo ya afya ya uzazi na uzazi wa mpango.

- Watoa huduma katika Kliniki za afya ya uzazi (RCH) wanashauriwa kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa kujifungua kwenye kituo cha kutolea huduma za afya na kutambua dalili za hatari kipindi cha ujauzito.

- Mkoa utaendeleza ushirikishwaji wa wanaume katika swala la afya ya uzazi na kuwajengea uelewa juu ya matumizi ya njia za kisasa za uzazi wa mpango.

### 3.6 Elimu

a. Ujenzi wa Bweni na Madarasa mawili (2) shule ya Sekondari Kasingirima

   - Fedha iliyotolewa kwa ajili ya ujenzi wa majengo hayo ni shilingi milioni 120 kutoka mradi wa EP4R tangu mwezi Juni mwaka 2020. Vyumba viwili vya madarasa vilitengewa shilingi milioni 40 na ujenzi wa bweni moja lenye kuchukua wanafunzi 80 unagharimu shilingi milioni 80.

b. Ukarabati wa shule ya Sekondari Kigoma/Ujiji

   - Mradi huu wa ukarabati wa shule ya Sekondari Kigoma/Ujiji ambayo awali ilijulikana kama shule ya msingi Kigoma umetekelezwa kwa kutumia mapato ya ndani ya Halmashauri. Ukarabati huu umegharimu kiasi cha shilingi 124,588,800/=. Mradi unatekelezwa kwa njia ya Force Account kwa kutumia mafundi wa ndani chini ya usimamizi wa wataalam kutoka Ofisi ya Mhandisi wa Halmashauri ya Manispaa Kigoma.

   - Idadi ya vyumba vya madarasa vilivyojengwa katika shule za msingi imefikia 2095 mwaka 2020. Aidha, idadi ya vyumba vya madarasa katika Shule za Sekondari imefikia 1018.

c. Uandikishaji rika lengwa la watoto wa darasa la Elimu ya Awali umeongezeka kutoka asilimia 65 mwaka 2020 hadi asilimia 77 mwaka 2021.

d. Uandikishaji lengwa la watoto wa Darasa la Kwanza umefikia asilimia 99 mwaka 2021.

e. Ufaulu wa Wanafunzi waliojiunga na Kidato cha Kwanza umefikia asilimia 85 mwaka 2021.

f. Ufaulu wa kumaliza Elimu ya msingi umefikia asilimia 77.4 kwa takwimu za mwaka 2020. Aidha, ufaulu wa Kidato cha nne umeongezeka kutoka asilimia 83.01 mwaka 2019 hadi asilimia 89.48 mwaka 2020.

### 3.7 Maji

- Mkoa kupitia Wizara ya Maji na ufadhili wa Umoja wa Ulaya (European Union) na Serikali ya Ujerumani kupitia Benki yake ya Maendeleo ya KfW, inajenga mradi wa kuboresha huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji kwa gharama ya Shilingi **Bilioni 42.**

- Mradi huu unaotegemewa kukamilika ifikapo Aprili 2022, utaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 20 hadi kufikia lita milioni 42 kwa siku wakati mahitaji ya maji kwa sasa ni lita milioni 23. Kwa takwimu za **Sensa ya Taifa mwaka 2012** wakazi wa Manispaa ya Kigoma-Ujiji walikuwa **215,458** na kwa ongezeko la idadi ya watu kwa mwaka la asilimia **2.4**; kwa sasa wakazi wanakadiriwa kufikia **254,368**. Mradi huu ukikamilika utaweza kuhudumia idadi ya wakazi wapatao **384,501** sawa na kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa asilimia mia moja.

- Vilevile, mradi umelenga kuboresha huduma ya uondoaji wa majitaka kwa kujenga mabwawa ya kutibu majitaka yenye uwezo wa kuchukua mita za ujazo **160** kwa siku.

- Mradi wa Maji Kibondo Mjini unaotumia Kisima cha Twabagondozi umekamilika na unatoa huduma ya maji. Miradi mingine iliyokamilika ni Zashe, Mabamba/Mkarazi, Mukabuye, Kijiji cha Nguruka, Kijiji cha Uvinza, Nkuba na Keza, Kijiji cha Kwaga, Kijiji cha Samvura – Bunyambo, Churazo/Kinyinya/Nyanzige, Bukirilo, Gwarama na maeneo mengine.

- Upatikanaji wa huduma ya maji Vijijini ni asilimia 67 wakati Vijiji vinavyopata huduma ya maji ni 196 hadi sasa.

- Aidha, Mkoa kupitia Wakala wa Maji Vijijni (RUWASA) utashughulikia tatizo la maji Kidahwe – Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma. Kwa mujibu wa RUWASA Wilaya ya Kigoma, mradi huu umepangwa kukamilika kwa awamu mbili (2). Awamu ya kwanza ni kutoa maji kutoka kwenye chanzo, kupeleka kwenye tenki la maji na kusamabaza maji kwenye vituo 20. Kazi hii imetengewa kiasi cha Shilingi 700,000,000/= katika mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia mradi wa PforR (Programme for Results). Awamu ya pili imepangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo RUWASA Wilaya ya Kigoma itatenga kiasi cha Shilingi 700,000,000/= kwa ufadhili huo huo kwa ajili ya kupeleka maji kwenye *Treatment Unit*.

- Kwa mujibu wa RUWASA Wilaya ya Uvinza, mradi wa maji katika kijiji cha Mwakizega ambao umesimama kwa sasa, umepangwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwa kuwa mradi huo umewekwa kwenye bajeti kwa ajili ya kuukamilisha kwa kutengewa kiasi cha Shilingi 475,000,000/= kwa ufadhili wa Benki ya Dunia (World Bank) kupitia mradi wa PforR (Programme for Results).

- Pia, Mkoa utaendelea kumkumbusha Mheshimiwa Waziri wa Maji kuunda Bodi ya Maji Wilayani Kibondo.

### 3.8 Taarifa ya Mikopo ya Asilimia 10 iliyotolewa kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Juni, 2020.

- Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Juni, 2021 Halmashauri zote nane (8) za Mkoa Kigoma zimefanikiwa kutoa mikopo yenye tahamani ya Shilingi 835,466,722.83/= kwa Vikundi 156 vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu. Vikundi 91 vya Wanawake vimepata Shilingi 451,775,817.06/=, Vikundi 44 vya Vijana vimepata Shilingi 262,827,929.14/= na Vikundi 21 vya Watu wenye Ulemavu vimepata Shilingi 109,062,239.39/=. Mchanganuo wa fedha hizo kwa kila Halmashauri ni kama inavyoonekana hapa chini.

| Halmashauri | Fedha za asilimia 10 (Jul 2020-Juni 2021) zilizotengwa (TZS) | Jumla ya mikopo tolewa kwa kipindi cha Jul 2020 - Juni 2021 (TZS) | % ya mikopo iliyotolewa | Fedha tolewa kwa vikundi | | | Idadi ya vikundi vilivyokopeshwa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Wanawake | Vijana | Watu wenye Ulemavu | KE | VIJ. | WU | Jml |
| Buhigwe | 78,818,489.20 | 61,300,000.00 | 77.8 | 48,000,000.00 | 9,500,000.00 | 3,000,000.00 | 13 | 3 | 1 | 17 |
| Kakonko | 52,487,089.85 | 58,000,000.00 | 110.5 | 24,000,000.00 | 16,000,000.00 | 8,000,000.00 | 4 | 3 | 2 | 9 |
| Kasulu DC | 188,440,988.24 | 170,797,795.00 | 90.6 | 74,130,000.00 | 74,667,795.00 | 22,000,000.00 | 18 | 14 | 5 | 37 |
| Kasulu TC | 137,133,453.23 | 135,923,061.00 | 99.1 | 71,423,061.00 | 33,550,000.00 | 29,950,000.00 | 14 | 6 | 4 | 22 |
| Kibondo | 153,802,926.96 | 145,031,129.59 | 96.7 | 101,222,756.06 | 31,696,134.14 | 12,112,239.39 | 21 | 6 | 3 | 30 |
| Kigoma DC | 55,414,737.23 | 55,414,737.24 | 100.0 | 36,000,000.00 | 7,414,000.00 | 12,000,000.00 | 8 | 1 | 3 | 12 |
| Kigoma MC | 199,475,228.30 | 85,000,000.00 | 42.6 | 49,000,000.00 | 34,000,000.00 | 2,000,000.00 | 7 | 5 | 1 | 13 |
| Uvinza | 135,746,694.66 | 124,000,000.00 | 91.3 | 48,000,000.00 | 56,000,000.00 | 20,000,000.00 | 6 | 6 | 2 | 14 |
| **JUMLA** | **1,001,319,607.65** | **835,466,722.83** | **83.4** | **451,775,817.06** | **262,827,929.14** | **109,062,239.39** | **91** | **44** | **21** | **156** |

### 3.9 Ulinzi na Usalama

- Hali ya usalama inaendelea kuimarika licha ya kuwepo kwa matukio machache ya uhalifu. Matukio ya uhalifu katika eneo la Kibondo hivi karibuni (kuteka basi la abiria) yalisababisha upotevu wa mali za Wananchi. Vitendo hivi vinaendelea kudhibitiwa na jeshi la Polisi.

## 4.0 Changamoto na Utatuzi wake

Pamoja na Mafanukio tuliyoyapata Kisekta katika kipindi cha mwaka mmoja wa Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, changamoto kubwa zifuatazo zimejitokeza na utatuzi wake uko katika hatua mbalimbali kama inavyooneshwa katika Bangokitita Na.4.0

Bangokitita Na.4.0: Changamoto na Utatuzi wake

| Na. | Changamoto | Utatuzi | Hatua iliyofikiwa |
|---|---|---|---|
| 01. | Ugonjwa wa Homa kali ya Mapafu unaosababishwa na Virusi vya Korona umeendelea kuathiri Mkoa na nchi yetu kwa ujumla. Hadi kufikia tarehe 24/02/2021 Mkoa ulikuwa na jumla ya wagonjwa 72 waliothibitika kimaabara tangu kuanza kwa mlipuko huu. Wagonjwa hawa wanatoka katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Halmashauri ya Wilaya Kigoma, Kibondo na Halmashauri ya Mji Kasulu. | Mkoa umeendelea kuchukua hatua na tahadhari mbalimbali kukabiliana na kudhibiti kuenea kwa Mlipuko huo hatari ndani ya Mkoa. | Mpaka zoezi la utaratibu wa karantini ya lazima unasitishwa Tanzania, jumla ya Wasafiri 340 walipitia karantini zilizopo ndani ya Mkoa. |
| 02. | Mitaji midogo kwa Mawakala wa Mkoa wa Kigoma husababisha baadhi yao kushindwa kuleta pembejeo za kutosha. | Mkoa unaendelea kuwahamasisha Wafanyabiashara wa pembejeo za Kilimo kuongeza mitaji yao na kuleta pembejeo kwa wingi na kuzipeleka kwa wakulima. | Pamoja na mitaji midogo kwa Mawakala wa Mkoa Kigoma, upatiakanaji wa mbolea kwa wakulima unaridhisha. |
| 03. | Upungufu wa Umeme | Jitihada mbalimbali zinaendelea kufanyika ili kuhakikisha umeme unapatikana kwa wingi kwa kuanzisha miradi ya kuzalisha umeme. | Hivi sasa Kigoma tunapata umeme wastani wa 1MW kutoka kituo cha kuzalisha Umeme kwa kutumia nguvu ya jua (Solar Plant Power). Kituo hiki kinaendelea kufanyiwa maboresho ili kitoe umeme zaidi. |

## 5.0 Miradi inayotekelezwa na itakayotekelezwa 2021/2022

### 5.1 Mradi Mkubwa wa Maji Manispaa Kigoma/Ujiji

Mradi huu unaotegemewa kukamilika ifikapo Aprili 2022, utaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 20 hadi kufikia lita milioni 42 kwa siku wakati mahitaji ya maji kwa sasa ni lita milioni 23. Kwa takwimu za **Sensa ya Taifa mwaka 2012** wakazi wa Manispaa ya Kigoma-Ujiji walikuwa **215,458** na kwa ongezeko la idadi ya watu kwa mwaka la asilimia **2.4**; kwa sasa wakazi wanakadiriwa kufikia **254,368**. Mradi huu ukikamilika utaweza kuhudumia idadi ya wakazi wapatao **384,501** sawa na kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa asilimia mia moja.

### 5.2 Barabara

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, TARURA Mkoa wa Kigoma umepangiwa kiasi cha Shilingi Bilioni 6.386 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara katika Halmashauri zote nane za Mkoa wa Kigoma. Fedha ambazo zimekwishapokelewa hadi sasa ni Shilingi Bilioni 2.151 sawa na asilimia 33.68. Hadi sasa jumla ya Mikataba 31 imeshaingiwa na Wakandarasi wako hatua za mwanzoni kuanza kazi.

## 6.0 Hitimisho

Mkoa umeendelea kutekeleza kikamilifu Ilani ya Uchaguzi ya chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020, Ilani ambayo imetuagiza kuendeleza mapambano dhidi ya umasikini, ukosefu wa ajira, rushwa na kudumisha umoja, amani, ulinzi na usalama.

Mafanikio yaliyopatiakana kwa kipindi hiki yamechangiwa na ushirikiano na mshikamano uliopo kati ya Serikali ya Mkoa, Uongozi wa Chama cha Mapinduzi na Uongozi wa Serikali katika ngazi za Wilaya, Tarafa, Kata, Vijiji/Mitaa na Vitongoji.

Matarajio ya Serikali ngazi ya Mkoa ni kuona utekelezaji wa Ilani unaendelea kwa kasi kutegemeana na upatikananaji wa rasilimali fedha pale zinapohitajika. Ongezeko la Watumishi katika Sekta za Utawala, Afya na Elimu litachochea zaidi kasi ya utekelezaji wa Ilani.

CGF (Mst.) Thobias E. Andengenye
**Mkuu wa Mkoa**
**KIGOMA**